

JIELIMISHE KUHUSU UGONJWA WA HOMA KALI YA MAPAFU UNAOBABISHWA NA KIRUSI CHA CORONA

JINSI YA KUJIKINGA



Nawa mikono kwa maji



Funika mdomo na pua



Kaa mbali na mtu mwenye mafua au kikohozi ambaye
ana historia ya kusafiri nje ya nchi

AFYA YANGU MTAJI WANGU!

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto,
Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma

Na: 645

@elimu_ya_afya

@elimuyaafya

@elimu_ya_afya

@Afya TV Online



JIKINGE NA WAKINGE WENGINE DHIDI YA MAGONJWA

Nawa mikono yako kwa maji tiririka na sabuni:



- Baada ya kukohoa au kupiga chafya
- Baada ya kumhudumia mgonjwa
- Kabla na baada ya kuandaa chakula
- Kabla ya kula
- Baada ya kutoka chooni
- Baada ya kushika mnyama au kinyesi cha mnyama

AFYA YANGU, MTAJI WANGU!

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto,
Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma

[@elimu_ya_afya](#) [@elimuyaafya](#) [@elimu_ya_afya](#) [@Afya TV Online](#)

Na: 620



CORONAVIRUS

Coronaviruses havina kinga wala tiba

ila hutibiwa kutokana na dalili
anazoonesha Mgonjwa

NJIA ZA KUPUNGUZA MAAMBUKIZI



Ziba mdomo ukikoho
au kupiga chafya



Nawa Mikono kwa
Maji tiririka



Usipeane Mikono



Usishirikiane vitu
na Muathirika




Kaa mbali na Watu
wanaokoho na kupiga Chafya



Safisha sehemu
zinazogusa sana na Watu

DALILI ZA MARA KWA MARA ZA CORONAVIRUS



Homa

Kikohazi Kikavu baada
ya siku 2-7

Kupumua kwa tabu

Kukosa hamu ya kula

Kuharisha

Maumivu ya Mwil
kwa Ujumla

DALILI ZA MARA CHACHE

- Homa ya Mapafu
- Homa Kali
- Kukhoa Damu
- Figo Kushindwa kufanya
kazi

Utangulizi

Homa kali ya mapafu inasababishwa na Virusi vya 'Corona' ni ugonjwa unaoambukizwa kwa kuingiwa na majimaji yatokayo kwenye njia ya hewa wakati mtu mwenye ugonjwa huu anapokoho au kupiga chafya. Njia nyingine ya maambukizi ni kwa kugusa majimaji yanayotoka puanī (kamasi), kugusa vitambaa au nguo zilizotumiwa na mta mwenye maambukizi ya ugonjwa huu, au maeneo mengine yaliyoguswa na mta mwenye Virusi vya ugonjwa huu.

DALILI ZA HOMA YA CORONA



Homa na Matua Makali



Kikohazi



Kubanwa mbavu na
kupumua kwa shida



Mwili Kuchoka



Maumivu ya Misuli



Vidonda kooni



Kuumwa Kichwa

Matibabu

Ugonjwa huu hauna chanjo wala tiba ya moja kwa moja, hivyo kama yalivyo magonjwa mengine yanayosababishwa na virusi, matibabu hufanyika kwa kuzingatia dalili zilizopo na ufuutiliaji wa karibu.

Jinsi ya kujikinga na homa ya Virusi vya Corona

- Kaa mbali na mtu mwenye dalili za mafua mwenye historia ya kusafiri katika nchi zenyetlipuko wa ugonjwa huo
- Funika mdomo na pua wakati wa kukohoa kwa kutumia kitambaa safi au sehemu ya mbele ya kiwiko cha mkono au nguo uliyovaa sehemu za mikono
- Epuka kugusana na mgonjwa mwenye dalili za mafua au kikohozi
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono, kukumbatiana au kubusiana
- Epuka kugusa macho, pua au mdomo
- Subiri au epuka safari zisizo za lazima kwenda kwenye maeneo yaliyo athirika na inapolazimu kusafiri pata maelezo ya kitaalamu kabila ya kuondoka nchini
- Nawa mikono kwa maji yanayotirinka na sabuni mara kwa mara
- Ukiona mojawapo ya dalili za ugonjwa huu, wahi kituo cha huduma za afya
- Vile vile toa tarifa kwenye kituo cha huduma za afya uonapo mtu mwenye dalili za ugonjwa huu au piga simu namba

0800110124 au 0800110125 bila malipo.



Kumbuka ugonjwa huu haupo nchini Tanzania, hata hivyo kutokana na mwingiliano mkubwa uliopo hasa kibashara na kijamii kati ya Tanzania na nchi nyingine ni muhimu kuchukua tahadhari ili kuzuia usiingie nchini.